TANGAZO la Serikali Na. 357 la tarehe 26/4/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(Sura ya 272)

AMRI

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ("MASWA WSSA"), MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA. 2019

Jina

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa ("Maswa WSSA"), ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira, 2019.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Mei 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za maji safi na ada za Maswa WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.…

Masharti

4.-(1) Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 31 Agosti, 2019 au kabla, Maswa WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii.

(b) Maswa WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii. ®

(c) Maswa WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la

Amri hii.

(d) ifikapo tarehe 30 Juni, 2018 au kabla, Maswa WSSA itahakikisha inawafungia wateja wote wasio wa majumbani dira na wateja wote kufungiwa dira ifikapo au kabla ya tarehe 30 June 2020.

(e) Maswa WSSA ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kisheria kukusanya tozo ya udhibiti ya EWURA na kuiwasilisha EWURA.

(f) Maswa WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne.

(g) Maswa WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA.

(2) Taarifa hzilizowasilishwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Maswa WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake

(3) EWURA itazingatia tathmini iliyofanywa kwa mijibu wa aya hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Maswa WSSA katika siku zijazo.

Kufuta Amri Na. 11-004 la tarehe 1 Juni 2011

5. Amri hii inafuta matumizi ya Amri Na. 11-004 ya tarehe 1 Juni 2011, katika maeneo yanayohudumiwa na Maswa WSSA.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

	Bei za Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
Kundi la Wateja	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	445	1,100	1,600	1,900
Biashara	655	1,600	2,300	2,800
Taasisi	550	1,300	1,900	2,400
Viwanda	1035	2,400	2,600	2,900
Magati	1000	1,100	1,600	1,900
Wastani Linganisho	487	1,188	1,710	2,049

Jedwali Namba 1(b): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/ Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	5,500	17,600	25,600	Bei ya wasio na dira hairuhusiwi
Biashara	9,500	32,000	Bei ya wasio na dira hairuhusiwi	
Taasisi	11,500	26,000		
Viwanda	50,000	240,000		
Magati		Bei ya wasio na dira hairuhusiwi		

Jedwali Namba 1(c): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo Ya Sasa	Tozo Zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	500	Tozo ya Huduma Hairuhusiwi		
Biashara	1,000			
Taasisi	1,000			
Viwanda	1,000			
Magati	NA			

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	-	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Majisafi za mwaka 2013		
Biashara	-			
Taasisi	-			
Viwanda	-			
Magati	-			

Jedwali Namba 1(e): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada za sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	5,500	10,000	10,000	10,000
Biashara	5,500	10,000	10,000	10,000
Taasisi	5,500	10,000	10,000	10,000
Viwanda	5,500	10,000	10,000	10,000
Magati	5,500	10,000	10,000	10,000

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA (SHILINGI KWA MILIONI)

Maelezo ya uwekezaji mpya, mabadilisho ya miundombinu na ukarabati	2019/20	2020/21
Kubadili dira zilizoharibika 200	20	
Kununua dira 1550 kwa wateja wasio na dira	170.89	
Kununua dira 1,051 kwa wateja wapya	115.87	
Kununua dira kubwa 3 kwa ajili ya vyanzo vya maji na matanki		3
Matengenezo ya bomba kuu		
1 km GRP daraja C, kipenyo 16"	4	
1 km GRP daraja C, kipenyo 14"	4	
0.9 km GRP daraja C, kipenyo 12"	4	
Kununua pikipiki 6	6	6.27
Jumla ya gharama ya uwekezaji	324.76	9.27

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2018/19	2019/20	2020/21
Kiwango cha upotevu wa maji	%	45%	40%	35%
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato (bila madeni)	%	80	85	90
Kiwango cha ufungaji Dira	%	65	100	100

JEDWALI LA NNE
MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI MILIONI)

Gharama	2018/19	2019/20	2020/21
Uzalishaji	50.66	131.41	132.42
Umeme kwa ajili ya uzalishaji	365.49	441.18	444.61
Usambazaji	2	2.25	2.25
Matengenezo	8.31	83	828.75
Watumishi	107.22	139.56	146.6
Utawala	117.13	129.13	140.5
Matangazo	2.5	2.88	2.88
Matukio	6.5	6.5	6.5
Bodi	17.2	21.92	21.92
Fedha	1	1	1
Jumla ya Uendeshaji na Matengenezo	678.01	958.83	1,727.43
Gharama za Ukarabati na Uwekezaji		324.76	9.27
Jumla ya Mahitaji ya Fedha Requirement	678.01	1,283.59	1,736.70
Ondoa Fedha zingine zisizotokana na mauzo ya maji	12.45	22.88	10.81
Mahitaji ya fedha yanayotokana na mauzo ya maji	665.56	1,260.71	1,725.89

Dodoma,
11 Aprili, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY,
Mkurugenzi Mkuu